

## SERA YA MATUMIZI BORA YA TECHIE KIT

TANGIBLE INITIATIVES FOR LOCAL DEVELOPMENT TANZANIA (TIFLD) ni Shirika lisilo la Kiserikali na linalojiendesha kwa maudhui na njia za Tehama kwa kufanya kazi za kusaidia kupunguza na kumaliza umaskini, kuleta usawa wa makundi mbalimbali ya kijamii , kuchangia maendeleo ya sera, sheria za kukuza kanuni za demokrasia na uwezo wa kitaasisi. Shirika linaamini katika kujenga jamii za kuhimili utulivu ili kuendeleza maendeleo kupitia njia shirikishi na zenye ubunifu.

Katika kufanikisha utume wake na maono TIFLD inaendesha mfumo wa kimtandao unaojulikana kama Techie Kit ambao unakusudia kuwapa waandishi wa habari fursa ya kujua masuala muhimu yanayohusu tasnia ya habari kwa haraka na kwa urahisi. Kwa kuamini, kuzingatia na kudumisha ushiriki salama na wenye manufaa kwa mtandao na washiriki wote ambao wanajiunga na techie Kit, washiriki wanakubali kufuata sheria na kanuni kama zinavyoafikiwa wakati wa mshiriki kujisajili;

(i) **Uwasilishaji wa hoja zenye ukweli.** Washiriki watahiriki na kutoa hoja zenye utafiti wa kweli kama ilivyoonekana katika eneo fulani au mada ya ushawishi katika Techie Kit. Hairuhusiwi kutumia majina bandia na habari isiyo na hoja au tafiti inayojitosheleza. Mshiriki ana wajibu wa kufanyia utafiti wa kutosha kwa hoja yake kabla hajashirikisha katika Techie Kit.

(ii) **Mada za majadiliano.** Washiriki katika hoja za Techie Kit watazingatia mada mahsusi wakati wa kutoa hoja na ushiriki bila kutoka nje ya mada husika.

(iii) **Heshima ya maoni ya kila mshiriki.** Washiriki watatendeanza kwa heshima na kwa usawa. Mshiriki haruhusiwi kufanya shambulio la kibinafsi katika Techie Kit, na kila

mshiriki ana haki ya kuripoti chochote ambacho amekwazika kwa muongozaji wa Techie Kit.

(iv) **Heshima mtandaoni.** Ni marufuku katika Techie Kit kutumia mabavu, machafuko, ponografia, matusi, au kutishia maneno au huduma yoyote ambayo inakiuka haki za wengine kama hakimiliki, alama ya biashara, hati miliki, faragha au umma au vinginevyo ambavyo vinakiuka sheria.

(v) **Marufuku ya matangazo.** Hairuhusiwi kutuma tangazo ndani ya Techie Kit isipokuwa kwa ruhusa ya TIFLD na hiyo ni iwapo tu ni kwa faida ya jamii. Machapisho ambayo yana biashara, kampeni au ushawishi nje ya maudhui ya Techie Kit hayaruhusiwi.

(vi) **Nguvu ya Muongozaji wa Techie Kit.** Msimamizi wa Techie Kit atakuwa na ilani na nguvu wakati wowote wa hoja , uwasilishaji zaidi wa hoja, kufunga hoja au kuzuia uwasilishaji zaidi wa hoja. Msimamizi atakuwa na haki ya kufuta, kuhariri hoja au kuchapisha tena hoja katika Techie Kit au uwezo wa kumpiga marufuku mshiriki katika Jukwaa wakati inahitajika kufanya hivyo.

**Kwamba,** washiriki wa Techie Kit wanawajibika kwa yote wanayoweka kwenye Kit. TIFLD watakuwa na haki, lakini sio jukumu la kusahihisha makosa yoyote au kutolewa kwa yaliyomo katika hali yoyote kama watakavyoona inafaa na kupendeza kiulinganifu.

**Kwamba,** Techie Kit ni fursa kwa wanahabari kujua masuala muhimu kama sheria na sera za habari nchini na pia ni fursa kwao kuwa na mijadala inayojenga na kamwe sio mahali pa kukiuka sheria yoyote au kujadili shughuli haramu.